Kikao kilianza majira ya saa mbili kamili, timu nzima ilikuwepo, Husein, Peter na Paulo, Hadija Zaburi, Gaudensi, Asha na Mzee Makunja.

Kilikuwa kikao cha menejimenti ya Arusha Tanzanite Company Ltd, na ajenda kuu ilikuwa jinsi ya kuimarisha ukusanyaji wa madini na kudhibiti madini yasiyo na kiwango kwenda kwenye masoko ya nje ya nchi kwa kushirikiana na serikali.

Waliafikiana kwanza kuchakata wazo ndani ya kampuni kisha walipeleke kwa mdau mkubwa yaani serikali.

“Moja kati ya changamoto za hawa wafanyabiashara wadogo ni kukosa vifaa vya utambuzi wa ubora, ndio wamekuwa wakitumia njia za asili lakini bado zimewagharimu, hivyo unaonaje ikiwa tutaweka taratibu ya huduma ya bure ya upimaji wa awali?” Gaudensi aliendelea kutema cheche.

“Hilo sio jambo baya, ila sasa ukumbuke hiyo sio misingi ya biashara yetu, hivyo naafiki mwanzo wa wazo lako ya kuwa tushawishi na kununua sisi ila sasa ni vyema kujua zoezi hili linafanyika lini?” Husein alihoji.

Majadiliano yalidumu kwa muda na mwisho, ulifika muda wa kupiga kura ili kufanya maamuzi juu ya wazo la Gaudensi, mzani wa kura ulisimama kati kati kwani mzee hakuwa rasmi katika menejiment hivyo hakupiga kura. Mzee Makunja alitumia kura yake turufu kuamua na hivo wazo la Gaudensi lilipita, moja kwa moja ikiwa sheria.

Baada ya kikao Gaudensi alitumia muda ule kuaga juu ya safari yake ya kwenda Angola.

“Mimi ninaenda Angola, lakini nitarejea siku chache baadaye, hata hivyo shughuli nyingine nitaanza kwa njia ya mtandao.” Gaudensi alimueleza Mzee Makunja.

***

Haikumchukua muda mrefu katika safari yake nchini Angola, hivyo alirejea na kuendelea na kazi kwa kasi ya ajabu. Alikuwa kama simba mwenye njaa na sasa ameona kundi la swala. Kwa muda mfupi kampuni ilianza kushamiri.

Kipindi hiki ndipo Gaudensi aliweza kutumia ujuzi wake vyema na kwa uhuru. Baba alianza kukabidhi majukumu yake kwa Gaudensi. Gaudensi alianza kung’aa. Mzee alimpa gari mpya ya kutumia na stahiki zake nyingi.

Akiwa katika shughuli za kila siku alianza kuelewa mambo mengi ya Arusha Tanzanite. Ndani ya muda mfupi aliweza kubaini madudu kwenye idara ya manunuzi na maeneo mengine. Gaudensi hakusita kutoa ushauri japo mara kadhaa aligonga ukuta.

Moja ya mambo magumu ilikuwa suala la msuguano baina ya kampuni ya Arusha Tanzanite na wachuuzi wadogo wadogo ambao kwa jiji la Arusha wana sehemu kubwa ya soko la madini na wamekuwa wakivuka nchi za jirani kuuza madini. Serikali

imepambana bila mafanikio kwani njia za panya zilishamiri karibu kila pande.

Baada ya muda jambo hili lilipata mwelekeo, ilikuwa matunda ya ushauri wa Gaudensi.

“Nashukuru kwa wazo lako, tumeanza kupokea mzigo, si haba” alikuwa mzee Makunja akiongea na Gaudensi.

“Ondoa shaka baba, hiyo ni sehemu tu ya kozi yangu niliyoisoma” Gaudensi alimjibu baba yake.

“Unajua hawa wachuuzi wana tabia ya kwenda kwa mtu anayewajali hata kama bei sio nzuri ila utu kwao ni silaha kubwa. Sasa hatua itakayofuata ni kuwapa vifaa vya kupimia madini ili nao wayapime walau kwa hatua za awali ili kutambua na kujiridhisha kabla hawajaleta kwetu, baba mkifanya hivyo mtakuwa mmewasaidia wao kununua madini ambayo hayatawapa hasara na hivyo watazidi kuwa karibu na sisi.” Alihitimisha.

Ushauri wa Gaudensi juu ya kuwaendea washindani uliendelea kurindima kwenye akili ya Mzee Makunja, aliona nuru juu ya masuala ambayo yalishaanza kuwa kama saratani kwenye kampuni. Aliona wazi kabisa kuwa sasa kampuni itapata mwelekeo.

Upande wa pili mambo hayakuwa shwari. Mara tu Peter na Paulo walipoingia ofisini kwa Makunja, Makunja alilipuka na kumvaa

Peter kwa maneno, ilikuwa dhahiri kuwa alikuwa na lake lililomsibu kwa muda mrefu.

“Peter niliwaagiza wewe na mwenzako mnipe taarifa juu ya hizi faini tunazopigwa kila mara na watu wa mapato, enh! Inakuwaje wakati nimekuwa nikiidhinisha fedha chungu tele? Ina maana huwa hazifiki kwa wahusika?” Mzee Makunja alilalama kwa Peter wakati huo huo ni kama alitaraji yeyote ajibu kwa kuwa wawili hawa ndio waliokuwa wakiendesha kampuni kama viongozi wa ngazi za juu kwa takribani mwaka toka Mzee aamue kuwapa nafasi akijaribu kukaa pembeni kuona ikiwa wataweza kuendesha kampuni.

Kabla ya kungoja jibu toka kwa Peter na Paulo, Mzee alinyakua faili lililoandikwa barua za nje na kulibwaga mezani huku akionesha barua ya onyo toka mamlaka ya mapato.

“Ona hii barua ina mwezi haijajibiwa, Enh! Peter unategemea nani aijibu? Kwani wewe sio mkuu wa idara ya fedha, Ehn!”

“Baba haya mambo yanakwenda taratibu sio kama unavyodhani, isitoshe hiyo ndiyo kwanza barua ya kwanza bado pana onyo la pili na tatu ndio labda hatua zichukuliwe” Paulo alijaribu kumtuliza Mzee Makunja.

Kitendo cha kutochukulia umakini, ama umuhimu nyara ya serikali kilimkera mno Mzee Makunja akajikuta akiachia lugha kali.

“Upuuzi kabisa, ama kweli sasa naanza kuona madhara ya kufanya kazi bila taaluma ya kutosha! Hivi huoni kama hii ni dalili mbaya? Kwanini itokee kipindi majukumu yapo kwenu? Kampuni imeendeshwa kwa miaka chungu tele bila hati chafu leo kuwakabidhi nyinyi hata mwaka bado tayari mna barua ya onyo?” Mzee alitua.

“Lakini baba...” Kabla Paulo hajafika mbali na maoni yake, Mzee Makunja alimkatiza.

“Kelele...tena wewe ndio ovyo kabisa, umefanya manunuzi ya vifaa vibovu na kwa gharama kubwa, umetia hasara.” Mzee alimkatiza kwa ukali.

Mzee Makunja sasa aliona kiti ni cha moto alinyanyuka akifoka huku anazunguka chumba kizima.

“Ona nilikuwa na Gaudensi hapa tunapitia faili la manunuzi na wazi kabisa inaonesha kampuni iliyo-supply vifaa ni kampuni ambayo haina vigezo, na nakumbuka idara ya manunuzi walitoa tahadhari juu ya kufanya kazi na kampuni ya Kanjanja Entreprises! Sasa iweje bado mliwapa kandarasi? Mbona naona wanangu ndio mnahujumu kampuni? Kuna nini kinaendelea hapa, ehh?”

Peter na Paulo walikuwa kimya kama wamemwagiwa maji. Ukimya ulitawala kidogo huku Mzee Makunja akihema kwa jazba. Wakati bado wanatazamana, kila pande ikijaribu kuwaza jinsi ya kurudi katika maongezi ambayo dhahiri yalianza kupoteza mwelekeo, mlango ulifunguliwa, Asha aliingia katikati

ya kikao. Asha alileta faili lenye taarifa ya wachunguzi wa madini, na moja kwa moja lilipokelewa na Mzee Makunja.

“Ehe! Nyinyi watoto mtaniua, hawa pia wametuandikia kuwa sampuli zote zilizoenda hakuna hata moja iliyofikia viwango! Na haya niliyategemea, loh! Asante Gaudensi, sijui aliona nini ila amenipa suluhisho ya kuwa hawa wachuuzi wadogo wadogo tuwape vipimo vile vya awali na naona ni wazo mujarabu maana nikiendelea kuwasikiliza nyinyi haki hii biashara itakufa.” Mzee alitua na kushusha pumzi ndefu.

Hasira za Mzee Makunja zilitulizwa na simu iliyoita mezani, ilimbidi kurejea kwenye kiti chake na kuipokea, moja kwa moja aliipeleka sikioni huku akiwaonesha ishara Peter na Paulo kuwa watoke ofisini kwake.

Kufumba na kufumbua alibaki Asha, ambaye alikuwa akimtengenezea chai. Mzee Makunja alikuwa mraibu wa chai.

“Hallow...bwana Khalfan!”

“Habari, za siku mbili tatu” Khalfan alikuwa upande wa pili wa simu.

Baada ya maneno machache Mzee Makunja akikata simu kisha alimgeukia Asha.

“Niandalie kikao na bwana Khalfan pamoja na wakili Msomi Magoda, watakuja kesho mapema. Hakikisha umeandaa taarifa zote za mwaka, nahitaji kuzipitia pamoja nao maana kuna

mambo siyaelewi kabisa, huu ni muda wa kupata ushauri juu ya haya yanayotokea" Aliweka tuo.

"Sawa Baba, vipi kuhusu suala la gari ya bosi Gaudensi ambayo ulisema tuiagize toka Japan? Leo nimepokea barua pepe kuwa inatarajia kuwasili baada ya siku ishirini na moja." Asha alimkumbusha Mzee Makunja.

"Nakumbuka, hiyo utaenda kwa Peter umwambie afanye malipo yote na ikatiwe bima kubwa kisha itaegeshwa nyumbani, hiyo ni ya kazi maalumu."

Asha aliafiki maelekezo kisha akatoka nje akimuacha mzee akinywa chai.

Mara kadhaa katika vikao vya kampuni ambavyo Gaudensi ameshiriki alihoji juu ya mifumo ya udhibiti wa matumizi huku akionesha nia ya kampuni kutumia washauri wabobezi katika biashara.

"Unajua biashara zinayumba na hapana shaka tunahitaji mtu ama mawazo ya kutunasua lakini Peter na huyu Paulo wamekuwa wakimpiga vita huyu kijana mdogo Gaudensi, mimi sikuwa najua kwanini walikuwa wakipinga, ila kwa haya matokeo sasa naelewa vizuri hawa wana shida" Mzee alitua na kuwaacha washauri wake wachakate maelezo.

Makunja na washauri wake wachache waliona kuwa kesho ya kampuni ipo mikononi mwa Gaudensi, tofauti na timu ya Peter na Paulo wao hawakuwa pamoja na baba wala washauri wake.

Peter na Paulo hawakuamini uwezo wa Gaudensi, lakini pia walishajiwekea aina ya maisha ambayo bila kuwa na mzunguko wa matumizi ya juu basi hadhi yao ingeshuka, hivyo kwa kila namna walilazimika kupambana ili uongozi wa juu wa kampuni usibadilike na haswa usiangukie katika mikono ya Gaudensi, kwa kuwa alishaonesha nia ya kudhibiti mifumo.

Loh! Kwa hili walichelewa kwani imani ya mzee Makunja kwao ilimtoka, kwa kila hali alihamishia imani yake kwa Gaudensi, kweli alimaanisha hivyo.

Kwa kutumia wanasheria wa kampuni na washauri wa kampuni, taratibu za kisheria zilikamilishwa kwa Gaudensi kupewa hati maalumu ya kisheria iliyomuwezesha kufanya maamuzi mazito ya kampuni bila ulazima wa kupata sahihi za Peter na Paulo wala mzee Makunja, kazi ilibaki moja tu kwa Gaudensi kuthibitisha kuwa yeye ni msomi na hakurudi mikono mitupu bali mwenye uwezo wa kuiongoza kampuni kuifikia ile ahadi ya asali na maziwa.

Ndoto za mzee Makunja kuwa na kampuni kubwa katika ulimwengu wa madini ya vito ilitekelezwa vizuri na Gaudensi. Mzee alianza mapumziko ya nafsi na akili huku akishuhudia ukuaji wa Arusha Tanzanite Ltd. Muda wote mzee alitabasamu na kujivunia kijana wake yaani Gaudensi.

Ndani ya familia mapokeo juu ya madaraka makubwa aliyopewa na baba yake yaliwashtua nduguze, ndugu ambao walimzidi umri na uzoefu katika biashara ya madini lakini hilo halikuwa kikwazo

kwa baba, kumpa nafasi hiyo Gaudensi kwa kuwa aliwazidi nduguze elimu ya usimamizi wa madini, jambo ambalo baba aliamini Gaudensi angeongeza ufanisi wa biashara yao.

Familia ilikuwa katika mgogoro mkubwa, mgogoro uliopelekea kaka zake, kuamua kujitoa kufanya kazi na baba yao. Kampuni ya Arusha Tanzanite ilitikisika kiasi kutokana na kujitoa kwa watendaji wazoefu.

Baadhi ya masoko yaliponyoka, wafanyakazi wengine nao waliondoka sambamba na Peter na Paulo lakini muda mfupi baada ya Gaudensi kupewa mamlaka kamili, kampuni ilirejea katika ubora wake na kujipatia mafanikio makubwa kupita kipindi cha miaka kumi ya uendeshwaji wake, kipindi ambacho Gaudensi hakuwa yeyote wala lolote.

Mafanikio ya kampuni ya Arusha Tanzanite yaliiweka kampuni miongoni mwa makampuni matatu makubwa ndani ya kanda wa Afrika ya Mashariki.

Moja ya mafanikio makubwa chini ya uongozi wa Gaudensi Makunja ni kufungua matawi ya kampuni katika nchi ya Zambia na Rwanda na hivyo kuongeza mauzo ya vito kwa zaidi ya asilimia thelathini ndani ya muongo mmoja.

Miaka kadhaa iliyopita kampuni ilijaribu kujitanua katika nchi hizo hizo lakini iligonga ukuta mpaka alipoingia Gaudensi na timu yake ikitumia wataalamu mbalimbali wa tafiti za kitaalamu hadi kufikia lengo.

Japo haikuwa zoezi rahisi, maana ilitumika uwekezaji wa gharama kubwa tofauti na kipindi cha uongozi wa mzee Makunja akishirikiana na watoto wake wakubwa kwa Gaudensi.

Kipindi cha uongozi wa Gaudensi kampuni ilishuhudia kuongezeka kwa kundi la wataalamu mbalimbali wengine wakiajiriwa na wengine kupitia makampuni na taasisi za ushauri katika kila hatua ya uendeshaji wa miradi ya Arusha Tanzanite.

Kwa kuwa huu ulikuwa utaratibu mpya na uliotumia fedha nyingi, ni mzee Makunja pekee ndiye aliyetokea kuelewa na kuafiki akiamini katika uwezo wa Gaudensi huku watoto wake wakubwa wakiamua kujitoa kwa kigezo cha kutoafiki matumizi makubwa ya fedha kupitia kwa mdogo wao Gaudensi.

Kujitoa kwa kaka zake hakukumfanya Gaudensi kusita kutumia elimu yake na mipango madhubuti juu ya usimamizi wa madeni, hivyo aliendelea kushikilia uzi na kweli mafanikio yalionekana baada ya miaka michache kupita, kampuni iliweza kusimama kileleni ikichuana na makampuni ya kigeni tena yenye uzoefu na mitaji mikubwa zaidi ya Arusha Tanzanite.

Kufanikisha kukua kwa Arusha Tanzanite kuliingia sura mpya baada ya Peter na Paulo kurudi kwa mzee Makunja na kutaka mzee Makunja na bodi ya kampuni, kumng'oa Gaudensi katika nafasi yake kwa kigezo kuwa Gaudensi alikuwa mtu hatari kukabidhiwa majukumu makubwa na gawio kubwa ingali akiwa bado kapera na badala yake wao wapewe tena nafasi sio katika bodi tu bali mpaka maamuzi ya kila siku ya kampuni.

Ndugu wa Gaudensi walijipanga vyema na kupigilia msumari ya kuwa maamuzi makubwa yanahitaji utulivu na hali ya kujidhatiti, uwezo wa malezi na busara, huku wakisisitiza kuwa yote hayo hupatikana katika mtu mwenye ndoa na kamwe si kapera.

Hoja ya Gaudensi kuwa kapera ilipewa uzito sio tu na kaka zake bali hata ndani ya familia, mama Gaudensi, kama ilivyo kwa akina mama wengi wanavyotamani kuona watoto wao wakioa na kuleta wajukuu, wakati huo huo sera ya kampuni ilimtaka mtoa maamuzi mkuu wa kampuni kuwa mtu mwenye mke tena mke wa ndoa; jambo ambalo mara kadhaa lilimpa kigugumizi kijana Gaudensi kwa kweli katika hili Gaudensi alishikwa pabaya.

Si kwamba Gaudensi hakuwa na mahusiano la, ila hakuwa na mahusiano yaliyowahi kukubalika na familia yake.

Mpenzi wa kwanza kutambulishwa na Gaudensi kwa familia alikuwa raia wa Angola. Huyu alikuwa mtaalamu wa madini ambaye Gaudensi alimwamini kuwa ukiachia mbali mahusiano kama mke, Gaudensi aliamini angekuwa msaada mkubwa katika kuendesha na kustawisha biashara ya familia ya Makunja.

Tofauti na matarajio ya Gaudensi, penzi lao lilipigwa vita mapema asubuhi moja ya hofu kubwa iliyofanikiwa kulibomoa penzi la Gaudensi na mtoto wa Kiangola ni kuhusu jinsi ya kulinda biashara.

Timu ya mzee Makunja ikiongozwa na kaka wakubwa wa Gaudensi wakihofu siri za kampuni ya Arusha Tanzanite kuvujishwa kwa njia ya penzi la wawili hawa na kuangukia kwa

kampuni ya baba mkwe wa Gaudensi. Huku wakizidi kupigilia msumari kuwa mpenzi wa Gaudensi ni moja wa wamiliki wa kampuni ya madini ya Angola Meremeta Ltd.

Malaika kama ambavyo alifahamika kwa jina la kupewa na wazazi wake walikutana na Gaudensi pindi alipokuwa chuo cha madini kule Mererani kama moja ya wakufunzi wakifundisha somo la utafiti wa madini na Gaudensi alikuwa mmoja wa wanachuo pale chuoni.

Wawili hawa walianzisha mahusiano na kukubaliana ya kuwa, endapo watafunga ndoa basi ingemlazimu Malaika kuhamia Tanzania ili kujenga familia akiwa na mumewe Gaudensi. Suala la kuhamia Tanzania na kufanya maisha hapa liliafikiwa na Malaika kwa moyo mmoja kwa kuwa alimpenda Gaudensi na pia aliamini ya kuwa wangeendesha maisha yenye furaha na mafanikio.

Wakati wawili hawa wanapanga yao mchana, usiku wanga hawaruhusu hata lepe la usingizi nao wanapanga kuvuruga. Kwenye nuru penzi, kwenye giza vita na chuki alishafanya mawasiliano na kwao Angola. Baba yake alifurahi na kumuahidi zawadi kemkem tena akimuahidi kuwa ikiwa watafanikisha ndoa basi yupo radhi kutoa sehemu ya hisa zake na kumpa mkwe wake kama heshima na furaha ya kupata mkwe.

Habari zilimfikia Gaudensi naye akaamua kuziweka sirini na wawili hao wakaweka mpango madhubuti wa kuhakikisha watafanya makubaliano mazuri ya kuziwezesha kampuni zote mbili kubadilishana uzoefu kadhalika kuyafikia masoko

makubwa nje ya Afrika. Ama kwa hakika huu ungekuwa ukuaji wa kihistoria baina ya kampuni mbili ndani ya Afrika tokea nchi mbili tofauti kuunganika na kuishika dunia.

Maendeleo kama haya mara zote yameonekana baina ya mataifa ya weupe tu na katu hayajawahi kufikirika wala kutekelezeka ndani ya Waafrika na Waafrika wenyewe kwani Waafrika wengi wametawaliwa na uadui, chuki za wao kwa wao, tofauti kabisa na mataifa ya Ulaya, Asia na Amerika.

Ndoto za wawili hawa hazikuzaa matunda kwani katika hali isiyotarajiwa familia ya Makunja ilimkataa wazi Malaika na haikuwa tayari kumpokea Malaika kwa kuwa Malaika hakuwa na asili ya Tanzania tofauti na mila na desturi za kwao ambazo zinamtaka mtoto wa kiume wa mwisho kuzaliwa ni lazima aoe katika moja ya makabila ya jirani na asili yake ili muda wa uzeeni, makabila hayo yaweze kuendesha mila zao kwa urahisi ikiwa ni pamoja na kutembeleana kwa urahisi na hivyo umbali ungekuwa kikwazo.

Kwa kuwa Malaika alikuwa mgeni Tanzania tena akiwa hana usimamizi wa wazee wanaoweza kuzipambanua mila na desturi za Kitanzania, jambo hili lilimsikitisha, asiamini anayoyasikia hivyo alijikuta akipoteza matumaini ya kuwa na kijana kipenzi cha moyo wake, kijana Gaudensi.

Kwa upande wa Gaudensi, nduguze walimbana kwa kigezo cha kuwa Malaika kama alivyoitwa na wazazi wake, hakuwa mtu sahihi kuingia katika familia yao, kwa kuwa alikuwa shushushu

wa madini kutoka nchini Angola hivyo biashara yao ingekuwa hatarini kadhalika nchi nzima kwa ujumla.

Hoja hizi hazikuwa nyepesi hata kidogo. Mtu yeyote kwenye kutafakari mambo kwa kina ni dhahiri zingemgusa na kumfanya atafakari mustakabali wa ndoa yake dhidi ya nchi yake na hasa biashara yake. Njia panda juu ya nafsi yake ama wengi kama kiongozi ni jambo huweka kipimo cha utu na kujali wengine, kushinda mtihani huu hakika ni sifa kuu ya kiongozi, naam kiongozi hana budi kujitoa kwa wengine hususani wale anaowaongoza.

Gaudensi aliwaza, na kuamua kuiweka furaha yake pembeni ili aruhusu kuiokoa familia yake na biashara kwa ujumla. Japo kwa maumivu makali aliafiki kwa shingo upande akiheshimu na kuruhusu maoni ya nduguze dhidi ya jicho lake kwa Malaika.

Taarifa za kuwa familia ya Malaika ingetawala biashara za familia ya Makunja hazikuwa na mashiko kwani muunganiko wa kampuni mbili ungeweza kulindwa na mikataba na hivyo pande zote kunufaika.

Maskini kijana Gaudensi hakubaini kuwa lile lilikuwa zengwe, zengwe la kutengenezwa na nduguze wa damu, ili tu asimpate toka familia ya kitajiri tena tajiri kuliko familia yao.

Mafanikio ya kifedha na hitaji la moyo vilimsukuma Gaudensi kutupa karata yake ya pili kwa  mwingine. Safari hii akiwa na mahusiano thabiti na binti wa Kitanzania mwenye asili ya Kidigo toka mkoa wa Tanga.

Tanga mapenzi yalipozaliwa, ni Tanga hii hii ambayo baba yake Gaudensi alimpata mama watoto wake miaka arobaini na tano iliyopita na kufanya naye maisha na mpaka wanampata Gaudensi ambaye leo anarejea Tanga kufuata nyayo za baba yake.

Kama ilivyokuwa kwa baba, mwanae alipita katika njia za baba, Waswahili husema maji hufuata mkondo, Gaudensi alimpenda Janeth Mangara, mjukuu wa mzee Haji Mangara, mmoja wa mashujaa waliopigana vita vya mapinduzi kule Zanzibar; na baadae kupewa nafasi na heshima kubwa kama mashujaa wa taifa la Tanzania baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Gaudensi alisahau kabisa kuhusu Malaika wa Angola na sasa alitua katika penzi la mtoto wa Tanga. Mapenzi mapenzini, mahaba, mahabati, ndivyo ilivyokuwa kwa wawili hawa. Gaudensi sasa alizitumia siku za kazi jijini Arusha na siku za mwisho wa wiki alizitumbua jijini Tanga.

Ni kipindi hichi ambacho Gaudensi alipenda kwenda kwa wajomba zake ambao wengi waliishi jijini Tanga, kumbe kulikuwa na lake jambo, zaidi ya upwa na ujomba ambao kwa haraka ulijionesha kama sababu za safari zake.

## SEHEMU YA NNE

***"Simu ya mzee Makunja iliita na kumfanya aache kuongea na Asha ili apate kuipokea, ilikuwa sauti ya mwanamke, tena sauti ambayo haikuwa ngeni masikioni mwake"***

Janeth mcheshi, kifupi ni mwenye marafiki toka kila kona ya jiji la maraha Tanga; ni mwenye kutumia karibu asilimia sabini ya pato lake kujifurahisha. Hakuunyima moyo wake furaha aliamini ya kuwa raha jipe mwenyewe.
Janeth alijua haswa kujiachia, mpenda starehe, kwa kipindi hiki Gaudensi alihitaji mtu anayeweza kumsahaulisha maumivu ya mapenzi toka alazimishwe kuachana na Malaika kwa fitina za ndugu zake na kuandika upya ramani ya mapenzi katika hadidu za rejea za akili yake.

Pamoja na yote hayo, mapito ya miba na vichaka bado Gaudensi alipotezea ili kuulinda undugu wao, na kupiga moyo konde kuwa ipo siku atagusa pale ambapo yeye atafika huku akiamini na nduguze watamuelewa na kuwa upande wake, Gaudensi aliwapenda ndugu na hakuwahi kuwa na kinyongo wala husda dhidi yao, kwa kifupi alikuwa mtu wa moyo wa mtoto.

Uhusiano wa Gaudensi na Janeth ulianza kama masihara huku kila mmoja akimtambia mwenzie kuwa ana shida na anahitaji msaada.

Janeth alimuahidi Gaudensi kuwa angemletea mtu wa kumsaidia kumtuliza kwa kuwa alionekana anahitaji tulizo, alionekana ana moyo uliokonda, wenye hofu na masononeko ya mahaba.

Wakati Janeth anajiapia kuwa ana moyo wa kumsaidia Gaudensi, na Gaudensi alijitapa kuwa atamsaidia Janeth kumpata mtu sahihi ili asiendelee kuumizwa na mapenzi.

Wawili hawa wakajikuta wakiwa marafiki, watani, walioweka masihara kwenye urafiki wao urafiki ulioanzia kwenye ukumbi wa starehe pale jijini Tanga pindi Gaudensi alipoenda kujipumzisha kupata moja moto, moja baridi na kufurahia muziki mzuri toka Dj Sb aliyekuwa akipagawisha vizuri na kuwafanya wapenzi wa muziki kusahau shida zao walau kwa usiku mmoja.

Katikati ya muziki mnene, mkito mkubwa na mataa yanayowakawaka na kumetameta vyema na kuwafanya wapenzi wa muziki kupandwa wazimu, wazimu unaofuta hadhi ya mtu na hapo ndipo wote wanapokuwa sawa, katika muziki iwe tajiri iwe masikini ili mradi tu wote wanasikia sauti ya mikito inayodunda sambamba na hatua za uchezaji.

Muziki mtamu wa bongo fleva uliwakutanisha Gaudensi na Janeth, Janeth akiwa na chupa za mvinyo zisizopungua tatu tumboni mwake, mvinyo uliotulia vizuri juu ya vipande vya kuku vilivyotangulia muda mfupi uliopita. Ulikuwa mvinyo uliopeleka salamu kwenye kichwa na kumfanya kufurahia maisha kana kwamba hakukuwa na maisha zaidi ya haya.

Hii ilikuwa baada ya kazi na mikikimikiki ya jiji la Tanga kupita na hivyo kuukaribisha muda muafaka wa kumwagilia moyo, na hapo ndipo alipo Janeth alipoutendea haki moyo wake, alipenda muziki labda kuliko kitu chochote, kwake muziki ulikuwa starehe tosha, usipomkuta klabu ya muziki basi utampata kwenye bendi zinazopiga *live* na haikuwa ajabu kwake kupanda jukwaani na kuimba na kuserebuka sambamba na wana bendi.

Na ungemkuta kwenye jukwaa la bendi, Janeth huyu huyu wa Gaudensi ni mpaka mtu akutonye kuwa yule ni shabiki la sivyo waweza kudhani ni mmoja ya wana bendi, hana kasoro, toka sauti mpaka sare ya kucheza miondoko fulani, vyote Janeth alivimudu.

Katikati ya muziki majira ya saa tisa usiku, Gaudensi alijikuta mbele ya Janeth wakisakata dansi. Katika sauti ya kilevi Gaudensi alimsifia Janeth kwa umahiri wa kucheza japo Janeth hakusikia vizuri, kilichosemwa na Gaudensi lakini alihisi kuwa Gaudensi alipagawa na miondoko yake.

Baada ya nyimbo mbili tatu Janeth alimuaga Gaudensi kwa ishara kuwa anaenda kupumzika na Gaudensi alimjibu kwa ishara pia kuwa amefurahi kucheza naye.

Baada ya Janeth kuondoka, Gaudensi alivamiwa na wadada watatu na kuendelea kusakata dansi. Wadada walimzunguka kama mtu wanayemfahamu muda mrefu.

Mmoja aliingia na bilauri yenye mvinyo na kumnywesha Gaudensi, muda mfupi alijisogeza mlinzi na kuwataka waache

kunywa kinywaji ndani ya eneo la kucheza maana ni hatari kwa usalama wao, kwa kuwaelekeza kuwa endapo kinywaji kitamwagika basi sakafu inaweza kuuvaa utelezi na mtu kula mwereka, walimuelewa naye akashika yake.

Baada ya muda mchache kupita Gaudensi alitoka na kutafuta sehemu ya kukaa na kuendelea kunywa. Meza aliyokaa alizungukwa na wale mabinti, hivyo waliendelea kufurahi pamoja.

Akiwa mezani kwake Gaudensi aliweza kumuona Janeth na kumuagiza mhudumu kumpelekea kinywaji, bila kukosea mhudumu alifika alipo Janeth na kumtaka ajue hitaji la kinywaji chake ili apate kumhudumia.

Janeth alipojua kuwa amenunuliwa kinywaji na yule jamaa aliyekuwa anacheza nae muda mfupi uliopita, alimshukuru yule dada na kumtaka radhi ya kuwa alitosheka na vinywaji ambavyo tayari vilitabarizi tumboni mwake na hivyo asingeweza kuongeza kinywaji kingine asilani.

Mhudumu alirejesha majibu kwa Gaudensi kama yalivyotolewa na Janeth. Gaudensi akiwa na robo ya tabia yake ya mchana huku akili yake ikitumia asilimia sabini na tano ya nguvu ya mvinyo, alijikusanya na kufanikiwa kunyanyuka kwa mwendo wa kuyumba yumba na kumfuata Janeth.

Hatua za kilevi toka mezani pake mpaka kwa Janeth, tayari zilimpa nafasi mwanaume mwingine kufika na kuketi jirani na Janeth, kwa kifupi tu ni kwamba, Gaudensi alimkuta jibaba

mmoja akiongea na Janeth na kwa kuwa viti vilikuwa viwili tu, ilimpasa Gaudensi kusimama huku akimuongelesha Janeth.

Gaudensi bila kujali ni nani aliyeketi na Janeth, aliinama na kuongea na Janeth nusura aangukie meza ya Janeth lakini alimudu kufikisha ujumbe wake kwa sauti ya kilevi na kelele kubwa ili kuushinda muziki uliokuwa ukikita kwa nguvu zote.

“Naondoka, nimelewa, kwaheri” Gaudensi alimudu kutamka, kisha alisimama huku akiyumbayumba na kuondoka.

Janeth alimuonesha Gaudensi ishara ya kumuaga, na Gaudensi alimpungia kwa mkono wa kuondoka. Gaudensi aliondoka na kuanza safari ya kutoka nje, alikubali kukana nafsi yake juu ya starehe pale ndani na kukubali kwenda kulala.

Akiwa anatoka aliongozana na mabinti wawili kati ya wale watatu waliopata kucheza naye muziki. Mabinti wale waliongozana naye mpaka kwenye maegesho ya magari sehemu aliyoegesha gari lake, wote walionekana kuzidiwa kilevi japo Gaudensi ilikuwa mara dufu, hajiwezi asilani wala kujimudu.

***

Bombo ni hospitali ya rufaa pale jijini Tanga, hospitali iliyo nje kidogo ya jiji la mapenzi, karibu na ufukwe wa Raskazone.

Siku hiyo hospitali ilizidiwa na wagonjwa waliolazwa, kutokana na majeruhi waliopokelewa usiku wa kuamkia Jumapili, majeruhi

waliotokana na ajali iliyohusisha mabasi mawili yafanyayo safari zake kati ya Tanga na Dar es Salaam.

Asubuhi majira ya saa tatu siku ya Jumapili kundi la madaktari bingwa walikuwa katika mzunguko wa kupita kwa wagonjwa ndipo Dkt. Janeth alipomwona Gaudensi akiwa amelala kitandani hajitambui, mkononi akiwa na dripu ya maji ikiteremka taratibu kwa kasi ya tone moja kwa sekunde tatu, kipimo ambacho ni halali kwa mtu mwenye mapigo ya moyo mwendo wa 80 kwa 120 ili kumfanya mgonjwa asipande mapigo kwa kasi na kumfanya ajisikie kichefuchefu na kumsababishia kutapika.

Janeth alipigwa butwaa na kumsogelea kwa karibu, kwa kuwa alipewa taarifa kuwa mgonjwa yule hakuwa na fahamu, moja kwa moja Dkt. Janeth aliomba jalada na kulipitia ili kujua shida gani iliyosababisha Gaudensi kuwa pale alipo, tena katika hali ya kutojitambua.

Jalada la Gaudensi, lilikuwa na maelezo machache ya kuonesha ya kuwa mgonjwa yule aliweza kutambulika kupitia vitambulisho vyake na uchunguzi wa awali ukionesha kuwa alipewa madawa ya kulevya.

Dkt. Janeth aliwaeleza jopo la madaktari wenzake kuwa jana usiku alikutana na yule mgonjwa katika ukumbi wa starehe na mpaka muda anaondoka waliagana akiwa salama japo alionekana kulewa pombe.

“Pole kaka vipi unajiskiaje ?”Ilikuwa sauti ya mmoja wa wauguzi wa kike waliokuwa wakiwahudumia katika wodi

aliyolazwa.

Macho ya Gaudensi yalianza kufunguka moja baada ya jingine, la kushoto lilitangulia taratibu huku la kulia likafuata, pumzi zilikuwa na nguvu kuliko hapo awali, naam fahamu zilianza kurejea japo bado hakuwa na uwezo wa kuongea ila viungo vilianza kuonesha ushirikiano. Aliweza kujitambua kuwa yupo hospitali. Mengi zaidi yalikuwa mbali na ufahamu wake, alihitaji muda ili kurejea fahamu zake.

Akitambua ya kuwa mgonjwa wake amepata fahamu, mwuguzi alimueleza ya kuwa aondoe shaka kwa kuwa yupo mahala salama na kuwa kuna daktari ameweza kumtambua na pia ameagiza ya kuwa pindi apatapo fahamu tu aitwe mara moja.

“Pole kaka, hapa upo Hospitali ya Bombo Tanga. Leo wakati madaktari wanapita kuangalia hali za wagonjwa kuna dokta alikutambua. Alisema ukipata fahamu aitwe aje kukona, vipi ungependa nimuite sasa?” Muuguzi alimueleza.

Gaudensi alitikisa kichwa akionesha kuwa angependa aitwe.

***

Arusha katika ofisi za Arusha Tanzanite, muda wa kikao cha menejimenti ya Arusha Tanzanite ulihitimu. Wajumbe wote waliwasili tayari kujadili mambo muhimu, ikiwa ni kikao cha nusu mwaka kikao kinachopitisha mambo muhimu ya kimkakati kwa nusu ya pili ya mwaka.

Katibu wa kampuni alihakikisha maandalizi yote muhimu yamekamilika. Kwa utaratibu wa kampuni yao wajumbe waliopokea mwaliko ukiwa na ajenda za kikao pia ilikuwa lazima kwa kila mmoja kuthibitisha ushiriki wake bila uwakilishi.

Mpaka muda wa kikao kinafunguliwa mjumbe mmoja muhimu ambaye pia ni mkurugenzi mtendaji wa kampuni na kwa minajili ya kikao hiki cha bodi yeye hushika nafasi ya kuwa katibu wa kikao, hakuwepo kwenye chumba cha mkutano.

Mwenyekiti wa bodi ambaye pia ni mkurugenzi mtendaji mstaafu mzee Makunja, yeye binafsi na kupitia ofisi yake alifanya jitihada zote za kumtafuta Gaudensi, bila mafanikio.

Taarifa ya mwisho ya kiofisi iliyotolewa na katibu mukhtasi wa Gaudensi Asha ni kuwa Gaudensi alikwenda Tanga kwa mapumziko ya mwisho wa wiki na alipanga kurejea siku ya Jumapili tayari kwa maandalizi ya vikao hivyo muhimu vilivyopangwa kufanyika siku ya Jumatatu katika ofisi zao.

“Asha, Gaudensi yuko wapi? Sisi sote tunamsubiri yeye na unajua kikao bila yeye…! Mh! sio sawa”. Mzee Makunja alionesha wasiwasi japo aliishia katikati akishindwa kujua aulize vipi.

“Maandalizi yote yapo sawa tokea wiki iliyopita hivyo naamini muda wowote toka sasa ataingia.” Asha alimjibu mzee Makunja.

Muda wote huu wajumbe walikuwa wakijadili mambo kadha wa

kadha kama sehemu ya maandalizi ya mkutano. Wengine wakizunguka zunguka na vikombe vya kahawa kuvuta muda ili Gaudensi afike na kikao kianze, kwani kila mmoja alitaraji muda si mrefu angefika.

Simu ya mzee Makunja iliita na kumfanya aache kuongea na Asha ili apate kuipokea, ilikuwa sauti ya mwanamke, na sauti ambayo haikuwa ngeni  masikioni mwake.

“Makunja, namtafuta mwanao toka juzi, simpati kwenye simu zake, leo si mna kikao cha menejimenti? Naomba mpe simu niongee naye.” mama Gaudensi aliongea bila kituo na mzee Makunja alikuwa kimya kumsikiliza na pindi alipotua tu, mzee Makunja alipata nafasi.

“Mke wangu, hata mimi simpati” Jibu la mzee lilikuwa la mkato.

“Unasema? Ina maana hata kikao cha bodi hajahudhuria?”

“Ndio tunamsubiri na hakuna taarifa zake” mzee aliongeza maelezo.

“Mh! Mbona sio kawaida, yaani asiwe hewani kwa siku zaidi ya mbili, tafadhali mtafute halafu unipe niongee naye kuna jambo nataka kusema nae,” Mama alimaliza kutoa maagizo akijua kabisa punde tu mzee atamuunganisha na mwanaye.
Hali ya sintofahamu ilimkumba mzee Makunja na tayari wasiwasi ulimfika, mara hii haikuwa swala la kiofisi tena bali suala la kifamilia maana mama Gaudensi tayari aliingilia kati akimtaka mzee Makunja kuingilia kati suala la Gaudensi

kutokuwa hewani kwa siku takribani mbili, jambo ambalo sio kawaida yake.

Kwa upande wa kampuni hali ilikuwa mbaya zaidi kwani mambo yalisimama. Kutopatikana kwa mkurugenzi mtendaji tena mpya ilikuwa jambo lisilovumilika.
Mtoto kwa mama hakui, mama alipokata simu kwa baba alipiga kwa Asha, napo majibu yalifanana na yale ya baba kuwa Gaudensi hakuwepo ofisini.

Ni kama mama hakumuamini Asha wala kumuelewa mzee, hivyo simu ya tatu na ya nne zilienda kwa kaka zake Peter na Paulo, nao pia wakiulizwa suala lile "*yupo wapi Gaudensi?*"

"Mama mwanao amekua, vipi umtafute kama mtoto mdogo? Isitoshe atakuwa na *hangover* kutokana na ulevi wake, kwani huna taarifa kuwa mwanao sasa ameanza kushika fedha tena kwa kiburi? Mi nafikiri upate muda wa kumpa mwongozo wa matumizi kabla hazijamuua," Peter alihitimisha na kukata simu ya mama yake.

Loh! Peter labda hakujua anaongea na nani au ni makusudi tu ili kumuumiza mama. Majibu ya Peter yaliurarua moyo wa mama, yalimfanya mama azidi kuchanganyikiwa badala ya kumpa ahueni, hakuna jibu hata moja lililotoa suluhisho la wapi alipo Gaudensi zaidi ya kuonesha kutojali kwa kutopatikana kwa Gaudensi.

Kwa mara nyingine tena mama alipiga simu kwa mzee Makunja na mara hii maongezi yalichukua sura mpya.

“Baba Gaudensi, nilikupa mtoto ufanye naye kazi na sio umpoteze, naona wewe na wanao hamumtakii mema mwanangu, yaani Peter wa kunikatia simu hata kabla sijamaliza kuongea?” Mama alilalama kwa mzee Makunja.

Mama alisikika akitweta kama mtu aliyekimbia umbali fulani bila maandalizi.

“Sasa basi ikifika saa sita mchana leo hajapatikana, wote mtajutia kauli zenu, hutosikia simu yangu tena nikihoji kuhusu Gaudensi na kampuni yenu, kazi njema.” Mama Gaudensi alihitimisha risala kwa mumewe.

Risala ya mama iliibua kikao cha dharura, kikao kilichowakusanya kwanza wadau wanne ndani ya chumba cha ofisi ya mzee Makunja kama sehemu ya dharura huku wajumbe wengine kadhaa wakiendelea kuvuta subira ndani ya ukumbi wa mikutano.

Kikao hiki kiliitishwa na mzee Makunja na kuhudhuriwa na Peter na Paulo, Asha na mzee Makunja mwenyewe, ajenda ilikuwa moja tu *Gaudensi yuko wapi?*

***

Ilikuwa siku ya kwanza ya juma, majira ya saa nne asubuhi ndani ya hospitali ya Bombo, Tanga safari hii sio wodi ya wagojwa tena bali katika ofisi ya Dkt. Janeth Mangara, maongezi kati ya mgonjwa Gaudensi Makunja na Dkt. Janeth yakiendelea, huku Gaudensi akiwa na fahamu za kutosha.

“Janeth, asante kwa msaada wako ningefia Tanga aisee!

“Pole naona wadada wa Tanga wamekukaribisha kwa mabalaa,” Dkt. Janeth alimkebehi Gaudensi.

“Tanga ovyo kabisa, hamna ukarimu kwa wageni badala yake mnawaua!
“Ishia hapohapo ukora wako ndio umekuponza, wewe aliyekuambia uvamievamie wanawake ovyo nani, utavamia mpaka majini, hii Tanga kaka loh!”

Gaudensi alimtazama Janeth, akataka aseme jambo ila akaishia njiani akiuchunga mdomo wake ila bado Dkt. Janeth aligundua.

“We sema tu. Mimi wala sijali, hata ukitaka kunitusi, ni hiyari yako ila vidonge vyako nakupa,” alitua.

“Tanga yote kama siyo majini basi majambazi, wanawake ovyo ninyi,” Gaudensi alisema huku anajaribu kusimama kutoka pale ofisini kwa Dkt. Janeth.
“Hebu keti, unaenda wapi sasa?”

“Nyumbani kwangu.”

"Kwako wapi, mbona makubwa, madogo yana unafuu unataka kutoroka ama." Janeth aliongea huku akimfuata Gaudensi ambaye alionekana kupepesuka.

"Maana kwanza hujapona, pili jalada lako limefunguliwa, kote polisi na hospitali, hapa mpaka upate ruhusa ndio utoke na isitoshe polisi bado wanakuhitaji ili kupata maelezo yako, ueleze vizuri madawa ya kulevya ulitumia na nani? Unalo hilo." Janeth alimpakia Gaudensi maneno kana kwamba ni watu wanaofahamiana muda mrefu.

"Umesema? Janeth, mimi natumia madawa?" Gaudensi alimaka.

"He! Sio mimi, ni ripoti ya uchunguzi inasema hivyo, sasa unabishana na vipimo? Tena katika hospitali ya serikali?"

Gaudensi na Janeth walitengeneza mahusiano ya urafiki wao katika masihara makubwa, haikuwa rahisi kujua ni muda gani na nani alikuwa *serious* au katika masihara ila kuhusu madawa Gaudensi alionesha kukerwa kidogo.

"Wacha ujinga wako, kwanza leo ni siku gani?" Gaudensi alimuuliza Dkt. Janeth.

"Haha! Unajitoa ufahamu ili nikuone huna kumbukumbu?"

"Hebu wacha utoto Janeth, leo ni siku gani?" Gaudensi alitilia mkazo swali lake.

Gaudensi alipata hisia kichwani mwake ya kwamba aliwiwa kutekeleza jambo kubwa, ila hakuwa na uhakika ni lini, muda

gani wala jambo gani, sasa kumbukumbu zake zilianza kurejea na kupanga makabrasha katika ubongo wake.

Dkt. Janeth aligundua jambo alipomwona Gaudensi anaumiza kichwa kuvuta kumbukumbu, alijua wazi kitakachofuata ni kichwa kuuma na kumletea madhara kiafya. Dkt. Janeth aliandika dawa na kumuita mhudumu ambaye muda mfupi alirejea akiwa na kijifuko cha dawa, kisha alimtaka Gaudensi waongozane mpaka kwenye gari yake walipanda na kuondoka.

“Kunywa hizi dawa, tumia maji hayo hapo utulize kichwa la sivyo utakuwa chizi sasa hivi.”

Dkt. Janeth alimpa dawa huku akitoa gari kwenye maegesho ya hospitali ya Bombo tayari kukatiza mitaa ya jiji la Tanga.

“Mbona sio dawa za kichwa ambazo nimezizoea?”
“Mchanganyiko wa madawa uliyopewa na wale malaya wako umeharibu mfumo wa ubongo kwa hivyo toka sasa hutakiwi kuumiza kichwa wala kuwaza mambo mazito kwa muda mrefu maana utapata madhara makubwa kiafya hususani afya ya akili,” Janeth alihitimisha.

Umbali wa takribani dakika kumi ulimfanya Gaudensi kupitiwa na usingizi na kumuacha Janeth akiongea peke yake, huku akikatisha barabara za jiji la Tanga.

Barabara ya kumi na moja ndipo aliposimama toka atoke kwenye lango la hospitali ya Bombo na hapa ni kwenye duka la kisasa la mahitaji super market. Dkt. Janeth aliacha gari ikiunguruma huku

Gaudensi akivinjari kiyoyozi ndani ya gari dogo ya chini, gari safi na inayonukia manukato ya karafuu.

Janeth aliingia na kununua mahitaji ya ndani, pia aliongezea mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya Gaudensi maana toka afikishwe hospitali hakuna mwenye taarifa zake hivyo hapakuwa na ndugu wala rafiki zaidi ya Dkt. Janeth.

Majira ya saa saba mchana tayari Dkt. Janeth aliwasili ndani ya nyumba yake maeneo ya Pongwe nje kidogo ya manispaa ya Tanga.

Moja kwa moja alipitiliza mpaka jikoni na kuandaa chakula cha haraka haraka, Janeth hakuwa wa kawaida katika mapishi, kama sio udaktari basi Janeth angestahili kuwa mmoja wa wapishi mashuhuri au hata mkufunzi wa vyakula vya nchi mbalimbali. Janeth hupika masaptasapta, mahanjumati na vingine vyote ambavyo unaweza kuita wewe ilimradi ufikishe ujumbe ya kuwa Janeth ni fundi, fundi wa mapishi.

Tanga jiji lilitoa wanawake wapishi bila ubishi na ndio asili, toka mapishi ya jikoni mpaka chumbani, iwe ni ukarimu basi Tanga ndio chuo, ukarimu tayari amelifuzu kujitofautisha kabisa na wale mabinti waliyoshindwa kurudisha fadhila kwa Gaudensi kijana mgeni Tanga na aliyewakarimu wao wenyeji badala yake walimuweka matatizoni.
Gaudensi alishtuka toka usingizini na kujikuta yupo chumbani akiwa amelazwa kitandani, kitanda cha binti Mangara ama wengine humuita Dkt. Mangara Janeth.

Gaudensi alishtuka kuona amebadilishwa nguo, tofauti na zile alizokuwa amevalia mwanzo. Wakati anavuta kumbukumbu na kutaka kujua kuwa yupo wapi, Dkt. Janeth aliingia na kumtaka aamke na ajongee mezani kwa ajili ya chakula.

"Gaudensi karibu, hapa ni kwangu, amka twende ukale, halafu unywe dawa tena," Dkt. Janeth alimueleza Gaudensi.

"Hapana Janeth, dawa za kwanza zilinipeleka hospitali, za pili chumbani kwako, za tatu si naweza kujikuta nipo chumba cha maiti?"

"Loh! Mwanaume huna shukrani hata kidogo, hayo ndio malipo ya wema wangu?"

Maneno ya Dkt. Janeth yalimfunga mdomo Gaudensi kwa maana yalimgusa na ni kipindi hiki ambapo ilimpasa kufuta kauli zake dhidi ya Janeth ili hali iwe shwari.

"Kumradhi Janeth, nisamehe rafiki yangu!"

Gaudensi alijishusha baada ya kugundua alikosea.
"Usijali Gaudensi," Janeth alitabasamu na kumkaribisha chakula.

Wakiwa mezani Gaudensi na Dkt. Janeth waliweza kuongea juu ya mkasa mzima uliomtokea Gaudensi, huku Gaudensi akijaribu kuvuta kumbukumbu ya tukio zima.

"Unaweza kukumbuka nini kilitokea hadi ukapoteza fahamu?" Aliuliza Janeth.

"Tukio la mwisho nakumbuka wale mabinti waliniomba lifti kuwa niwapeleke wanapoishi maana hawakuwa na usafiri." Gaudensi alianza.
"Mh! Kwahiyo uliwapeleka mpaka wapi?"
"Ninachokumbuka ni kama walikuwa wakibishana kabla hawajaingia kwenye gari, na wakati huo mimi nilikuwa tayari nimewasha gari, nawasubiri wao tu wapande …"
"Kwa hiyo walipanda au?" Dkt. Janeth alizidi kumdadisi.
"Hapakuwa na shida juu ya ombi lao, hivyo kama nilivyokuambia, mabishano yao sikuyaelewa ila pia sikutaka kuweka mkazo kuwafuatilia," Gaudensi alijibu.

Dkt. Janeth aliamua kumtorosha Gaudensi kutoka hospitali na kisha kumhifadhi nyumbani kwake kinyume na utaratibu maana Gaudensi alipaswa kutoa taarifa kituo cha polisi mara baada ya kupata fahamu ili vyombo vya usalama viweze kuchukua hatua ikiwemo kuendesha uchunguzi juu ya tukio lililomtokea na pia wajithibitishie bila ya mashaka kuwa sio tukio la kujitakia na ikiwa angeweza kulisaidia jeshi la polisi kuwapata wahusika.

Mahojiano yao hayakufika mbali kwa sababu Gaudensi alianza kuchukuliwa na usingizi kutokana na nguvu ya dawa aliyokunywa muda mfupi baada ya kula, dawa ambazo zina mchanganyiko wa dawa maalumu za usingizi ili kumfanya apumzishe ubongo wake. Hii ilikuwa ni sehemu ya matibabu yake kutokana na madawa aliyonyweshwa.

Dkt. Janeth alinyanyua simu janja yake kumpigia mkuu aliyemwagiza kazi, huyu alikuwa mpelelezi mkuu wa mkoa.

“Habari mkuu, ni Janeth hapa.”

“Ndio Dkt. Janeth, nimeona nambari, yako vipi? Unaendeleaje na vipi hali ya mtu wetu?” Alikuwa mpelelezi upande wa pili.

“Nzuri mkuu, amechangamka kidogo ila bado hana taarifa zozote muhimu, isitoshe tukio la dawa inaonesha halielewi wala hawajui wahusika. Najaribu kumchimba na ikiwa tutapata taarifa zozote muhimu basi nitahakikisha nazitumia vilivyo.”

“Sawa, nilipata picha mjongeo za pale hotelini, inaonekana, wale mabinti walimsaula kila kitu kisha kumtelekeza, ila gari tu ndo tuliikuta na ipo hapa polisi, ukiona yupo vizuri mlete afunge jalada kisha tumkabidhi aende zake, tuna mambo mengi ya kufanya kuliko kusumbuka na huyu aliyekaribishwa Tanga na vidosho.”

“Sawa namalizia kazi ndogo na yeye halafu kama yupo safi namleta pia kama ni mchafu nitawaita, mnajua cha kufanya.”

“Una siku moja tu, kukamilisha utaratibu ili tuwakabidhi kikosi kazi wawatafute wale mabinti, japo hapana haraka maadamu picha zao zipo tutaziweka katika mfumo na watapatikana kirahisi,” mpelelezi alihitimisha.

Dkt. Janeth alipokea maelekezo na kisha alikata simu na kurejea ndani kuendelea na mipango yake.

## SEHEMU YA TANO

***Uamuzi uliopitishwa ulijaa hisia za kibinadamu zaidi kuliko hesabu za kibiashara, kwa mara nyingine kampuni iliingia katika mgogoro mwingine, mgogoro uliojipenyeza hadi ndani ya familia ya mzee Makunja.***

Asha mdogo kwa umri, aliyekomaa kiakili na mwenye kuelewa vyema kazi za bosi wake Gaudensi. Tena akiwa mtu aliyeshiriki kikamilifu kuandaa taarifa nzima ya bosi wake, achilia mbali kuwa alishapata kufanya kazi na mzee Makunja pindi akiitumikia kampuni katika nafasi ya mkurugenzi mtendaji, sasa alikabidhiwa na mwenyekiti wa bodi kuwasilisha taarifa ya kampuni ya Arusha Tanzanite kwa siku ya kwanza na kisha mwenyekiti wa bodi kuwaomba wajumbe kuahirisha kikao kile muhimu mpaka taarifa ya kupatikana kwa Gaudensi zitakapopatikana.

Kutoka kwa Asha, wajumbe waliipokea taarifa ya maendeleo ya kampuni ili kujiandaa kuijadili katika vikao vitakavyofuata. Uamuzi uliopitishwa ulijaa hisia za kibinadamu zaidi kuliko hesabu za kibiashara, kwa mara nyingine kampuni iliingia katika mgogoro mwingine, mgogoro uliojipenyeza hadi ndani ya familia ya mzee Makunja.

Timu ya Peter na Paulo ilishutumu maamuzi ya mwenyekiti wa bodi mzee Makunja, ila jambo zuri ni kuwa safari hii kura ya

mama na mzee Makunja zote zilibariki ya kuwa uhai wa Gaudensi ulikuwa muhimu kuliko kikao, hivyo Peter na Paulo walikosa kabisa mtu wa kuwaunga mkono na hata walipojaribu kupenyeza maneno kupitia kwa Asha, pia hakuwa upande wao kwa namna yoyote ile.

Suala la Gaudensi kutopatikana katika mawasiliano lilichukua sura mpya kwa mzee Makunja na aliamua kuvunja ukimya, na kuliondoa suala hili mikononi mwa familia ili mamlaka nyingine zipate taarifa, kwa kuwa haikuwa kawaida hata kidogo kwa Gaudensi kutoweka katika hali kama ile.

“Mama Gaudensi! Hili sasa halivumiliki nakwenda kwa inspekta Dula Kigunde kwa ajili ya kutuunganisha na kule Tanga maana taarifa ya mwisho ni kwamba alikwenda Tanga kwa ajili ya mapumziko,” mzee Makunja alimueleza mama Gaudensi.

Wawili hawa walikuwa katika sonona kuu, mama hakuwa na nguvu tena ya kufoka bali alijiegemeza kwa mzee Makunja kama tegemeo pekee na faraja yake katika kipindi hiki kigumu kuwahi kuikumba familia.

“Mume wangu, hebu simama kama baba, siku nne mwanao haonekani na wewe upo tu hapa Arusha! Mimi nilitegemea umeshakwenda huku na kule kumtafuta au ndio mmeungana na hao wanao wenye roho mbaya?”

“Mama Gaudensi, mke wangu kipenzi, sio kwamba simjali Gaudensi ila katika umri wake hata mimi nilikuwa na siri zangu. Na sio kwamba kila jambo nililolifanya basi wazazi wangu

walilifahamu, la hasha! Kuna mengi nilifanya kwa kificho halafu wazazi niliwaarifu baadae, kwa hiyo hata Gaudensi huenda ana jambo, tuwe na subira tupate taarifa za Tanga halafu mengine yatafuata." Wakati mama na baba Gaudensi wanashauriana jinsi ya kutatua suala la mtoto wao, simu ya mama iliita.

"Shikamoo mama" alikuwa Asha.

"Marahaba mwanangu, hujambo?"

"Sijambo mama, vipi na wewe hujambo?"

Mama aliongea kwa sauti ya chini mno isivyo kawaida yake, iliashiria wazi kuwa hakuwa sawa na Asha alitambua wazi kuwa ni kuhusu suala la Gaudensi.

Asha alikuwa na taarifa muhimu za kumfikishia mama Gaudensi hivyo alijipanga vyema kisha akaanza kutiririka.

"Pole mama najua suala la Gaudensi linakupa tabu ila sio wewe tu, hata mimi na wengine sote tunaguswa, amini kuwa linatugusa sote japo kwako ni zaidi na sisi tunafahamu hivyo."

Asha alianzisha maongezi kwa namna hii.

"Asante mwanangu, maana ni wewe pekee ndio umenikumbuka japo kwa simu na kunifariji jamani mwanangu sijui kakumbwa na nini?" Mama alimaliza kwa masikitiko na sasa ilikuwa zamu ya Asha kusema neno.

“Mama nina taarifa nzuri kuhusu bosi Gaudensi …”

Kabla ya Asha kumalizia kusema mama alidakia.

“Enhe! Amerudi? Yupo salama? Naomba niongee nae, mpe simu…” mama hakumpa nafasi tena Asha kumpa hizo taarifa.

Kama ambavyo Waswahili husema ng’ombe wa maskini hazai, ni kweli, wakati Asha ameduwaa kwa jinsi mama alivyomtandika maswali badala ya kusubiri taarifa yenyewe toka kwake, kibaka wa simu za mkononi aliipitia simu ya Asha na kuinyakua kama mwewe anyakuavyo kifaranga cha kuku.

Asha aliona simu yake ikipepea na yule kibaka na wala asijue la kufanya, Asha alisahau kufunga kioo cha mlango wa nyuma wa gari yake tena upande uleule alioketi.

Kibaka alifanya tukio lile kwa ustadi mkubwa kwani alisubiri gari za upande wa foleni ya Asha ziliporuhusiwa na kuanza kuondoka tu ndipo na yeye aliikwapua, katika hali ile Asha aliishia kupunguza mwendo na hapo gari za nyuma yake zilimtatiza kwa honi kali zikimtaka aache kuweka msongamano na pasipo kujali.

Asha hakuwa na la kufanya hivyo alijikuta akiongeza mwendo ili kupisha kadhia ile ambayo huenda ingeweza kumsababishia ajali na hivyo kuwa janga juu ya janga.

Mama Gaudensi alichanganyikiwa pale alipoita na kuongea peke yake kwenye simu huku upande wa pili wa simu akikosa majibu,

mama akaamua kuikata na kuipiga tena ile namba ya Asha akiamini ni tatizo la kimtandao kuwa Asha hamsikii au yeye ndio hamsikii Asha; mama alipoipiga ile namba ya Asha simu iliita bila kupokelewa mara kadhaa na mwisho simu haikuweza kuita badala yake yalisikika maneno ya kukatisha tamaa.

"*Namba unayoipigia kwa sasa haipatikani, tafadhali jaribu tena baadae*." Kana kwamba haitoshi, ujumbe ule ulijirudia kwa lugha ya kigeni.

Jambo lilikuwa jambo, mama alishindwa kujizuia, aliangua kilio cha haja, kilio cha msiba wa mama wa Kitanzania pale apatapo taarifa ya msiba mzito dhidi yake ama akaribiapo nyumba ya mfiwa aliyempenda ama mtu muhimu kwake ama kwa mtu wake, mama alilia kweli, alilia kwa sauti kuu.

Moja kwa moja mama Gaudensi aliangukia katika mikono ya mumewe mzee Makunja na kupokelewa kwa upendo mkubwa na baada ya kutulizwa na kufutwa machozi ndipo mzee alipoanza kuhoji kulikoni.

Mishale ya muda huchelewa usiku wa deni na huchelewa pale jambo zuri litokee kwako. Kwa mama na mzee Makunja, Mungu alikuwa upande wao, katikati ya simulizi ya mama kwa mumewe kuhusu simu iliyopigwa na Asha, mlio wa honi ya gari ulisikika nje ya lango kuu la nyumba yao.

Nyumba nzima ilikuwa kimya sio wao wala wafanyakazi ndani mpaka walinzi kwa pamoja walikuwa wamekusanyika sebuleni kutokana na kilio kilichoangushwa na mama, wote waliingiwa na

hofu maana sio jambo la kawaida kwa mtu mzima kuangua kilio kwa sauti kuu.

Wakiwa bado sebuleni, sebule iliyo juu ghorofani mzee alimtaka mlinzi kwenda kuhakiki honi ile iliyopigwa na kumtaka amwarifu kwa simu kuwa ni nani aliyekuja kabla ya kumruhusu kuingia, ikiwa ni mtu wa pale au si mtu anayefahamika.

Pia alimtaka mlinzi wa pili kuimarisha ulinzi pia kuweka vinasa picha vyema katika maeneo mazuri ili kupata matukio yote yanayoendelea. Kwa wafanyakazi wa ndani aliwataka waendelee na majukumu yao ila pia aliwataka wasipokee simu yoyote wasiyoijua na badala yake wakimbie kumpelekea na kuipokea mbele yake. Nyumba nzima sasa ilikuwa katika tahadhari na taharuki kubwa. Bosi mtoto alikuwa ametoweka.

Lango kubwa lilifunguliwa na gari ndogo iliingia katika maegesho ya magari. Ilikuwa gari ya Arusha Tanzanite gari ambayo hutumiwa na Asha hakuna asiyeijua. Kwa kuwa Asha alifahamika vyema pale nyumbani kwa mzee hivyo mlinzi alimruhusu kuingia bila wasiwasi.

Ujio wa Asha ulikuwa faraja kwa mama na familia nzima ya mzee Makunja. Mama alikuwa wa kwanza kumuona Asha akiteremka toka kwenye gari yake kupitia kamera zilizowekwa na kuonesha maeneo mbalimbali ya pale nyumbani.

Mama alimwambia dada wa kazi ateremke haraka kumpokea mgeni na kisha ampeleke moja kwa moja sebule ya juu, mahali ambapo familia walikaa kujadili mustakabali wa Gaudensi.

Simu zilizokuwa zikiingia mfululizo zilimfanya mzee Makunja asimuone mgeni aliyeingia na kuanza mazungumzo na mama Gaudensi.

Muda wote mzee Makunja alikuwa anaongea na mkuu wa upelelezi wa jiji la Tanga, simu aliyopigiwa ili kupata uthibitisho juu ya mambo kadhaa yanayomhusu Gaudensi. Mzee aliongea na simu kwa sauti ya chini huku akizungukazunguka kwenye ushoroba pembeni ya maua yaliyopangwa kupendezesha nyumba kadhalika kuongeza hewa safi ndani ya jumba la kifahari la Makunja.

"Ndio, mh sawa, ndio," Alisema Makunja.

"Natuma vijana wangu sasa hivi, wawili kutoka hapo hapo Tanga naomba niwape namba zako ili uwape maelekezo na baada ya kazi tuwasiliane ili tuangalie tunawafanyaje na nahitaji waliohusika nipate kukutana nao ana kwa ana maana inaweza kuwa hujuma za kibiashara." Aliendelea kutoa maagizo.

Mzee Makunja alimaliza maongezi na kukata simu kisha alirudi sebuleni na uso kwa uso alikutana na Asha.

"Karibu Asha." Ilikuwa kauli ya mapokezi ya mzee Makunja kwa Asha.
"Asante, poleni nilikuwa na taarifa za bosi Gaudensi lakini pindi napiga simu kwa mama nikapata shida pale kwenye mataa ya Mianzini. Kibaka alinipora simu na kutoweka nayo, sikuweza kufanya lolote zaidi ya kuendesha gari niwahi kuja hapa

nyumbani ili nikamilishe kufikisha taarifa kwa mdomo maana ndio hivyo tena simu imekwenda" Asha alitua.

"Oh! Pole mwanangu" mzee alimhurumia Asha.
"Mungu mkubwa alipora na kukimbia, bora hakukudhuru" mama alidakia.
"Ehe! Umeongea na mama kuhusu hizo taarifa sio?"
"Ndio nimemueleza ya kuwa Gaudensi yupo Tanga na yupo salama na kwamba kuna mtu amempa namba zetu ili atupigie, huyo mtu ana namba zetu ila sisi hatuna nambari zake maana zimepotea kwenye ile simu iliyokwapuliwa" Asha alisema.
Mzee Makunja alifikiri kidogo kisha akawataka wamsikilize kwa makini.
"Asante Asha, umekuwa msaada mkubwa hasa katika kipindi hiki cha matatizo" mzee alianza.
"Upande wangu pia nimepokea habari nzuri, nimeongea na mtu muhimu wa usalama kule Tanga na tayari nimeagiza watu wangu waende kumwona, kwa hiyo ndani ya saa moja toka sasa tutaongea na Gaudensi moja kwa moja." Mzee aliweka tuo.

"Ila inashangaza mno, kama yupo salama kwanini asitutafute, ama ndio usalama wa mdomoni tu, huku mtu anateketea?" Asha alihoji.
Uso wa mama Gaudensi ulijawa na wasiwasi ni kama hakuridhishwa na taarifa ya Asha, japo aliipokea kama taarifa ya awali tu labda mpaka hapo atakapomsikia Gaudensi kwa kinywa chake, kwa jinsi hali ilivyokuwa hakuwa mtu mwenye utulivu kila mara alitaka kufungua mdomo na kuishia kushika tama, ni dhahiri ya kuwa hakuwa na amani.

***

Jijini Tanga Dkt. Janeth alikamilisha taarifa yake dhidi ya Gaudensi kisha aliituma kwa mkuu wake wa kazi, taarifa iliyomuelezea vyema Gaudensi na taarifa zake muhimu, taarifa alizozipata kupitia alama za vidole, vinasaba na mitandao ya kijamii. Dkt. Janeth alikuwa na simu janja maalumu yenye uwezo wa kukusanya taarifa za mtu.

Kipindi chote hiki Gaudensi alipokuwa katika usingizi mzito kufuatia dozi ya dawa za mapumziko, dawa alizopewa na Dkt. Janeth na kumpatia usingizi mzito Dkt. Janeth alifanikisha kujipatia taarifa lukuki na taarifa hizo ndizo zilizompa nafasi mpelelezi mkuu wa mkoa wa Tanga kuweza kuwapata Asha na mzee Makunja.

Mpelelezi alitumia sehemu ya taarifa alizozipata toka kwa Janeth kuwaondoa hofu jeshi la polisi kuhusu tukio la madawa ya kulevya yaliyokutwa mwilini mwa Gaudensi na kwenye gari ya Gaudensi kuwa ni jambo la kupandikizwa ili kupoteza ushahidi wa wizi uliofanywa na wale mabinti watatu siku ya Jumamosi alfajiri.

Baada ya saa sita za usingizi wa mfululizo Gaudensi aliamka na kumkuta Dkt. Janeth akiwa pembeni yake, ameketi kwenye kitanda kilekile alicholala huku Janeth akijisomea kitabu cha riwaya ya *MAPENZI YAMELOGWA*, riwaya iliyoandikwa na mshindi wa tuzo ya uandishi bora wa riwaya ya mwaka 2016 huyu ni, Hussein Wamaywa.

Dkt. Janeth na Gaudensi walitazamana kwa sekunde chache.

“Habari, daktari” Gaudensi alimsabahi Janeth kwa kuzingatia taaluma yake. Toka wafahamiane wawili hawa wamekuwa marafiki wakubwa kwa usiku mmoja.

Gaudensi, alikuwa katika ubora wa kiwango cha lami tena lami ya viwanja vya ndege vya kimataifa toka afya ya mwili mpaka akili, kwa kifupi alirejea kwenye ufahamu wake kwa asilimia tisini na tisa.

“Habari mgonjwa” ndilo jibu la salamu alilolitoa Janeth kwa Gaudensi.

Janeth  chotara wa Kidigo na Kingoni ambaye huuficha uzuri wake kwa uchakaramu na masihara leo Gaudensi kwa mara ya kwanza alipata kumtizama akiwa hana kilevi kichwani, mning’inio wala msongo wa mawazo ila tu deni la fadhila.

Gaudensi hakujua angelipaje deni la fadhila maana hapakuwa na makubaliano yoyote baina yake na Janeth wala kiwango cha kufahamiana kwao hakikutosheleza kuwa sababu ya Janeth kumhudumia kiasi kile.

Ndani ya sekunde chache Gaudensi aliwaza mambo mengi, ikiwa pamoja na jinsi walivyokutana na Janeth, jinsi alipomwacha pale *club* usiku na kuondoka na wale mabinti watatu, kisha habari yake inaruka na kuhamia hospitali halafu inaishia kuwepo kwake pale kwenye himaya ya Janeth tena akipata huduma nzuri hata kurejea ufahamu wake na kuwa Gaudensi.

Gaudensi kijana rijali toka familia tajiri na yeye mwenyewe akiwa mhimili wa utajiri wa familia yao, alitambua kuwa Janeth hakuwa rafiki wa kawaida tu, bali mwanamke aliyejitoa kuokoa uhai wake, mwanamke aliyempa deni la upendo, deni ambalo labda lingeweza kufidiwa na bima kama kungekuwepo na huduma hiyo duniani *bima ya penzi*. Gaudensi aliteremka kitandani na kupiga magoti.

Kipindi chote hiki Janeth alikuwa akimtazama mgonjwa wake huku akiwa na uhakika kuwa dozi alizompatia kwa taaluma yake zimetamatika hivyo Gaudensi yupo sawa na tayari kuyakabili majukumu yake kama mtu mwingine au kama ilivyokuwa hapo awali.

Janeth alipata hisia ya kuwa Gaudensi amepiga magoti kumshukuru Mungu wake kwa yote yaliyomtokea, hivyo Janeth alinyanyua kitabu chake cha riwaya na kuendelea kusoma akimwacha Gaudensi afanye jambo lake.

"Dkt. Janeth" Gaudensi alimuita bila ya kuhamisha macho toka kwenye kitabu alichokuwa anasoma, Janeth aliitika "Abee Gaudensi."

Kwa kuona kuwa Janeth hamjali, Gaudensi aliita mara mbili zaidi, kwa upole na staha kubwa. Naam Janeth aligeuza sura na kugongana na Gaudensi, uso kwa uso, macho kwa macho, na hili ndilo lilikuwa lengo la Gaudensi, kukutanisha sura zao.

"Asante kwa kila ulilonifanyia pokea shukrani zangu toka kwenye uvungu wa nafsi ya moyo wangu."

"Usijali Gaudensi! Sasa endelea kusali na mimi nasoma kitabu."

"Janeth! Sio kila apigae magoti basi husali, bali kila apigae magoti anamaanisha yupo chini ya yule aliyepigiwa magoti."

Gaudensi alianzisha ngojera zake.

***************

**Baada ya kuonja kidogo sasa unaweza kununua ili kuendelea kufaidi uhondo huu. Mwandishi pia ana vitabu vingine vingi tafadhali ngalia na ununue ufurahie.**